OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA
SHULE YA SEKONDARI YA KIPONZELO

Simu : 0754 –451090/0755972509

Kumb. Na. KIPSS/JI/VOL.03/5

JINA LA MWANAFUNZI _____
S.L.P _____
IRINGA.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIPONZELO WILAYA IRINGA MKOA WA IRINGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

1. **UTANGULIZI**
   Ninafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari ya Kiponzelo mwaka 2021. Shule ya Sekondari KIponzelo ipo katika kata ya Maboga yenye vijiji tatu Kiponzelo, Magunga na Makongati. Ipo umbali wa **km 21** kusini mwa mji mdogo wa **Ifunda** katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa. Kwa wanafunzi watokao nje ya kata ya Maboga, usafiri wa basi kutoka Iringa mjini unapatikana stendi kuu ya mabasi ya zamani ya mkoa wa Iringa kwa nauli ya **Tsh. 3000.**
2. **KUFUNGUA SHULE**
   Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021** saa **7.00** asubuhi. Kila mmoja lazima awepo wakati huo na kuitika jina lake. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021** (ndani ya siku saba). Ukichelewa hutapokelewa bila ya kibali toka kwa Afisa Elimu Mkoa.
3. **KUSAJILIWA RASMI**
   Kila mwanafunzi lazima ahakikishe kuwa amesajiliwa katika daftari maalumu la usajiri na kupewa namba ya usajili. Usipokamilisha maelezo haya **HUTASAJILIWA.**
4. **UNAPOKUJA SHULENI**
   Uje na barua hii pamoja na fomu zilizoambatanishwa zikiwa zimekamilishwa vyema. Fomu hizo ni;
   (a) Fomu ya mwanafunzi na mzazi kukubali nafasi ya kujiunga kidato cha kwanza.
   (b) Fomu ya kupimwa afya na daktari wa Serikali.
5. **MIHULA YA SHULE**
   Shule ina mihula miwili
   Muhula wa kwanza Januari-juni
   Muhula wa pili Julai- Desemba.
6. **MAHITAJI MUHIMU YA SHULE**
   - Ndoo **MOJA (01**) ya ujazo wa lita 10 kwa ajiri ya utunzaji wa mazingira.
   - Ream **MOJA (01)** ya karatasi aina ya photocopy **A_4** kwa mwaka kwaajili ya majaribio mbalimbali.
   - Fagio **MOJA(01)** (chelewa) kwa ajili ya usafi wa mazingira.

7. SARE YA SHULE

WAVULANA Suruali mbili, moja iwe ya **DAMU YA MZEE** na nyingine kitambaa cha **KIJANI KIBICHI** itavaliwa siku ya **ALHAMIS NA IJUMAA.**

i. Shati mbili nyeupe mikono mirefu.
ii. Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba na kung'arisha kwa kiwi .(Jozi mbili na kuendelea).
iii. Soksi ndefu nyeupe (Jozi mbili na kuendelea).
iv. Mavazi ya michezo (T-shirt za blue 02, bukta 02 na raba 01, tracksuit mojarangi ya blue bahari).
v. Suruali iwe pana yenye marinda manne ya kuvalia kiunoni.
vi. Mkanda mweusi upana usizidi inchi 1 ½. (Miwili).
vii. Sweta iliyokolezwa**S**hingo V. Tafadhari ziwe **MBILI** moja iwe ya **BLUE** na nyingine **DAMU YA MZEE KAHAWIA**.

WASICHANA

i. Sketi mbili mshono wa rinda box isiyo bana mwili (kitambaa kizito) yenye urefu unapitiliza magoti. Moja iwe ya **DAMU YA MZEE** na nyingine kitambaa cha **KIJANI KIBICHI** itavaliwa siku ya **ALHAMIS NA IJUMAA**.
ii. Blauzi nyeupe mbili mikono mirefu.
iii. Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba na kung'arisha kwa kiwi (jozi mbili na kuendelea).
iv. Soksi ndefu nyeupe. jozi mbili na kuendelea.
v. Mavazi ya michezo. (T-shirt za blue 02, bukta 02, skin tight 02 na raba 01).
vi. Rangi ya ijabu ifanane na shati la shule (kwa wale wanaohusika).
vii. Mahitaji mengine ya kutosha ya kisichana.
viii. Sweta yenye Shingo ya V. Tafadhari ziwe **MBILI** moja iwe ya **BLUE** na nyingine **DAMU YA MZEE KAHAWIA**.

8. MAHITAJI MENGINE MUHIMU YA MWANAFUNZI

i. Kalamu za kutosha.
ii. Daftari kubwa 10.
iii. Mkebe wa hesabu.

USHAURI: Mzazi/mlezi unashauriwa kununua walau kitabu kimoja kimoja kwa kila somo pamoja na kamusi ya **KIINGEREZA** kwenda **KISWAHILI** ili kukuza **UJUZI** katika **LUGHA YA KIINGEREZA** kwani ndoo lugha ya kufundishia.

9. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII (ZITEKELEZWE NA MWANAFUNZI IPASAVYO)

Shule ina endeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu namba **25** ya mwaka **1978** na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria namba **10** ya mwaka **1995.** Aidha, ina zingatiwa miongozo yote inayo tolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Tekinologia na Ufundi yenye dhamana na elimu nchini na ofisi ya Rais (TAMISEMI) yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi ya fuatayo mara baada ya kufika shuleni:

- Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana ratiba ya shule ni lazima.
- Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (evening preparation).
- Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa hapa shuleni.
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- Kutunza mali za umma.
- Unatakiwa kuvaa sare za shule kwa mshono uliokubaliwa na kwa wakati kama taratibu za shule zinavyoelekeza hasa;
    - Wakati wa masomo darasani
    - Safari zote za nje ya shule kwa jina la shule
    - Wakati wa kwenda hospitali
    - Wakati wa maandamano ya amani.
- Shule hii ni ya serikali kila mwanafunzi atambue kuwa akiwa shuleni hutakuwa tofauti na mwenzio kwa misingi ya kidini, kikabila, rangi,kikanda na kiuchumi.
- Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kujadili dini au siasa ya mwingine, wala hairuhusiwi kuwa na mjadala ya kidini au siasa hapa shuleni, ukiukwaji wa maelezo haya yatasababisha mwanafunzi kuondolewa shuleni.
- Mwanafunzi haruhusiwi **KUMILIKI AU KUTUMIA SIMU** au kuwa na **LAINI YA SIMU** kipindi chote awapo nje na ndani ya mazingira ya shuleni.

  IKUMBUKWE: Bodi kwenye kikao chake cha tarehe **17/7/2020** illifikia uamuzi kuwa, adhabu ya mwanafunzi kukutwa/kutumia **SIMU au** kuwa na **LAINI YA SIMU** mzazi atatozwa **TOFALI KUBWA 500.**

10. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE MWANAFUNZI

- Wizi,
- Uasherati, uhusiano wa kimapenzi, ubakaji, na ushoga,
- Kulawiti,
- Kutembelea majumba ya starehe**,**
- Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa Bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika,
- Kupigana au kupiga,
- Kuharibu kwa makusudi mali ya umma,
- Kudharau bendera ya taifa,
- Makosa ya jinai,
- Kuoa au kuolewa,
- Kutoa mimba,
- Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule,
- Kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu,
- Kukataa adhabu kwa makusudi,
- Kuwa na simu ya mkononi,

- Kuchelewa kufika shuleni baada ya shule kufungua na kutoroka kabla ya shule kufungwa,
- Kutohudhuria masomo darasani/utoro,
- Kutofanya mazoezi au mitihani ya masomo na kutega vipindi,
- Kiburi na ukaidi,
- Kufanya jaribio lolote la kutaka kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu,
- Kushiriki uhalifu, siasa, na matendo yoyote yale yanavunja sheria za nchi,
- Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, walezi na jamii kwa ujumla.

MWISHO, kabisa nachukua nafasi hii tena kukukaribisha sana hapa Kiponzelo Shule ya Sekondari na ni matarajio yangu kuwa ufikapo hapa utaitumia vema fursa hii muhimu uliyopata kuongeza maarifa kwa faida yako binafsi, jamii na taifa.

KARIBU SANA TENA SANA KATIKA SHULE HII

……
MWL DALLU, E. E.
MKUU WA SHULE

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA
SHULE YA SEKONDARI YA KIPONZELO

FUMU YA KUKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA KWANZA

(sehemu ya kwanza ya fomu hii ijazwe na mwanafunzi na sehemu ya pili ijazwe na Mzazi au Mlezi)

(Sehemu hii ijazwe na Mwanafunzi mwenyewe)

PICHA

Mimi ---------- (Mwanafunzi) kwa hiari yangu nakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha Kwanza katika Shule Sekondari Kiponzelo. Aidha, naahidi kutoshiriki/kuanzisha migomo, fujo na makosa ya jinai na nitafuata sheria, kanuni na taratibu za shule ipasavyo.

Jina la Mwanafunzi ----------

Sahihi ya Mwanafunzi----------

Tarehe ----/------/20----------

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA
SHULE YA SEKONDARI YA KIPONZELO

FOMU YA KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO YA SHULE
HABARI ZA MZAZI/ MLEZI
(Fomu hii ijazwe na Mzazi /Mlezi)

1. Jina kamili la baba----------
2. Uraia ----------
3. Kazi yake ----------
4. Jina kamili la mama ----------
5. Uraia ----------
6. Kazi yake ----------
7. (Jina kamili la mlezi (iwapo haishi na wazazi wake) ----------

   kazi na anuani ya mzazi/mlezi ----------
8. Mtoto anaishi na Baba tu, Mama tu, Wazazi wote au Mlezi (**KATA** yasiyohusika).
9. Dini ya mzazi/----------
10. Dhehebu ----------
11. Anuani kamili ya sehemu ambako mtoto atakuwa anakwenda wakati wa likizo---------

    ----
12. Mimi ---------- mzazi/mlezi wa……. nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi. Naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi, mwenye bidii na hivyo atakuwa ni mtoto anayefundishika kwa kuwa atakuwa mtiifu wa sheria na kanuni za shule.Nitakuwa tayari kuitika wito shuleni muda wote nitakapohitajika kwa ajili ya malezi ya mtoto wangu.

---------- ----------
Tarehe Sahihi ya Mzazi/Mlezi

MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE AND VOCATIONAL TRAINING
KIPONZELO SECONDARY SCHOOL
MEDICAL EXAMINATION FORM
(<u>To be completed by medical officer in respect of all new students</u>)

Full name ----------

Age ----------

1. Blood count (red and white) ----------
2. Urine examination ----------
   ----
3. School examination ----------
   ----
4. Syphilis ----------
   ----
5. T.B Test ----------
   ----
6. Ear test ----------
   ----
7. Eye test ----------
   ----
8. Spleen ----------
   ----
9. Abdomen ----------
   ----
10. Additional information or any other Physical, Mental, Hereditary of infectious diseases
    ----

    Treatment after examination

MEDICAL CERTIFICATE

I certify that the above concerned has been examined medically and found fit to pursue secondary education.

Signature ----------
Designation ----------
Station ----------

(Official stamp)
Date ---/----/20---------

NB: Fomu hii ijazwe na mganga katika hospitali inayotambulika na serikali baada ya kumpima mwanafunzi ipasavyo.